**Sikiliza na Ujifunze - Mazingira na Hali ya Hewa**
**09 - Destructive Fishing Methods… Mbinu Haribifu za Uvuvi**
**Text: Richard Lough**
**Redaktion und Idee: Johannes Beck**
**Translator: Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum vya Sikiliza na Ujifunze juu ya mazingira ambapo leo hii tutazungumzia kuhusu taathira mbaya ya uvuvi wa kutumia baruti kwa miamba ya matumbawe yetu. Huchukua karne nyingi kwa miamba ya matumbawe kujiunda lakini yanaweza kuharibiwa kwa pigo moja tu. Radionovela leo itawaelezea kile kinachotokea kwa maisha ya wanyama au viumbe hai wa baharini wakati miamba ya matumbawe wanayoyategemea kwa uhai wao yanapolipuliwa vipande vipande. Pia tutatupia macho aina nyingine za uvuvi wa uharibifu na kutambua juu ya dhima ya shani inayotimizwa na mabwawa ya mikoko katika makuzi ya viumbe hai wadogo baharini.

Hali kadhalika tutapata mawili matatu kutoka kwa mwandishi wa Radio Deutsche Welle nchini Kenya Richard Lough (anatamkwa Lock) kuhusu kwa nini ni muhimu sana kutunza miamba ya matumbawe baharini na je ulikuwa ukijua kwamba matumbawe hayo mara nyingine huitwa misitu ya joto ya baharini kutokana na kuwa na wanyama au viumbe hai wengi sana wa aina mbali mbali?

**Music – 0:30**

**SFX Waves … mawimbi…**

| | |
|---|---|
| **Monica:** | Hebu angalia … angalia maji safi ya rangi ya feruzi yanavutia sana… |
| **Moses:** | Unajua … mwishoni mwa juma lililopita nilikwenda kuvua na baba yangu. |
| **Monica:** | Siku zote nilikuwa nikifikiria kwamba lazima itakuwa inachosha kuvua kwa kutupa mshipi baharini |

… kwani pengine unaweza ukapata kitu na mara nyingine unaweza kuondokea patupu.

**Moses:** (Excitedly… kwa msisimko) Uvuvi wa aina hiyo kweli unaweza ukachosha… lakini sisi tunatumia baruti.

**Monica/Gladys:** (exclaims in horror… tamka kwa mshtuko) Hapana… hamkuwahi kufanya hivyo!

**Moses:** Tumefanya… na mlipaswa mkione kile tulichokipata tulikumba aina zote za samaki unaowajua wewe kuanzia jodari, nguru, ngisi, pweza na hata taa (laughing… Sauti ya kicheko) Tulikula vizuri na kushiba kwa kuvimbiwa hapo Jumamosi usiku.

**Monica:** (curiously… kwa udadisi) Lakini vipi hasa aina hiyo ya uvuvi inafanyika? Najua kwamba wanaita uvuvi wa baruti lakini vipi unaweza kulipua kitu ndani ya maji?

**Moses:** (laughing… kwa kicheko) Unakuwa hutumii kijiti hasa cha baruti…

**Monica:** Alaaa…

**Moses:** Kile tunachofanya …

**Gladys:** Ina maana tayari mmekwishawahi kufanya hivyo?

**Moses:** Ndiyo… tena mbona mara nyingi tu. Huwa tunatumia chupa zilizojaa baruti iliotengenezwa kutokana na potassium nitrate au shure … ni mbolea ya kawaida hiyo ambayo ni rahisi kuinunua.

**SFX - flapping sail …… sauti ya tanga linalopepea kwa upepo)**

**Moses:** Jamani hebu waangalieni wavuvi wale… ati bado ingali wanatumia mashua za tanga na nyavu… ndio maana hawapati samaki wengi. Nashangaa kwa nini wanatumia uvuvi wa aina hiyo!

**Gladys:** (indignatly…… kwa hasira) Moses… kwa sababu uvuvi wa baruti ni haramu! Na sio hilo tu bali pia unaangamiza miamba ya matumbawe yetu!

**Monica:** Lakini samaki hasa hapo huwa wanakufa vipi?

**Moses:** Ahhhh… kwa mujibu alivyonielezea baba yangu milipuko hiyo ya baruti husababisha mawimbi ya vishindo chini ya bahari ambayo hupasua vibofu vya samaki na kuwafanya waelee juu ya maji. Unaona enhh … ni rahisi mno!

**Gladys:** (clicking her tongue in disgust… akipiga kidoko ulimi wake kwa kuchukizwa) Moses, Moses, Moses …

**Moses:** Nini tena?

**Gladys:** Je umeangalia chini ya bahari na kuona uharibifu mnaosababisha kwa mfumo wa ekelojia baharini!

**Moses:** Hapana… kwani tunakuwa hatuna hata haja ya kuingia majini… huwa tunazirusha tu chupa baharini…

**Gladys:** Hivi karibuni nilikwenda kuzamia mbizi na kaka yangu John ambaye ni mvuvi. Alinionyesha mashimo makubwa kwenye mgongo wa bahari yaliosababishwa na milipuko. Alisema miamba ya matumbawe ilikuwa kama ufalme ulioko chini ya bahari ambapo maisha ya viumbe hai wa majini yalikuwa mazuri na ya kupendeza. Hivi sasa hauna kitu kinachoishi hapo. Twendeni tukamtafute John,

kwa kawaida anakuwepo upande wa chini wa ufukwe …

**X-fade into SFX – hauling nets onto beach sauti ya kukokotwa kwa nyavu mchangani……………….**

**Gladys:** Habari gani John …

**John:** Poa Gladys …

**Monica:** Uvuvi wako umekwendaje leo hii… mambo mazuri?

**John:** (sigh…… akitanafusi kwa majonzi) Hapana, mambo yalikuwa mabaya sana! Miaka michache iliyopita tulikuwa juu ya matumbawe… unaona pale mahala mawimbi yanapokatika … kama kilomita 500 kutoka hapa. Lakini sasa matumbawe yale yameharibiwa na inabidi tutafute maeneo mapya ya kuvua samaki…

**Gladys:** John unaweza kutupeleka kwenye matumbawe kwa mashua yako? Rafiki yetu Moses anataka kujifunza zaidi juu ya jinsi uvuvi wa baruti unavyoharibu matumbawe…

**John:** Uharibifu? Maangamizi lingekuwa neno bora zaidi hapo … Bila ya shaka nitakuwa na furaha kuwapelekeni…

**SFX outboard engine starts up…… sauti ya kuwashwa kwa engine ya mashua…**

**X-fade into SFX running outboard engine + SFX boat through water…… changanya na sauti ya mashua inayotembea baharini**

**John:** Wavuvi wengi wanaotumia baruti hawajui kabisa madhara makubwa yanayoletwa na vitendo vyao.

**Gladys/Monica:Tunakuelewa!**

**John:** Baruti hizo huua kila kitu sio tu samaki bali pia wanyama wengine wasioweza kuliwa wa matumbawe. Mara nyingi matumbawe hulipuliwa mara mbili, kwanza kwa ajili ya kuwauwa samaki wadogo, halafu tena kwa ajili ya kuuwa mijisamaki mikubwa kama vile papa ambao huwa wamevutiwa na vifo vya mkururo wa samaki.

**Fade out SFX running outboard engine .,….X-fade into SFX lapping water …. Ondowa sauti ya engine ya mashua kwa kuchanganya na sauti ya mawimbi madogo ya bahari….**

**Gladys:** (with sorrow… kwa masikitiko) Angalia sasa kile kilichobaki kwenye matumbawe…

**Monica** (puzzled… akionekana kubabaika) Lakini nilikuwa nikidhania kwamba miamba ya matumbawe ilikuwa ina rangi mbali mbali za kupendeza… ni rangi ya kijivu tu iliopo hapa.

**John:** Unajua vishindo vya mawimbi vinavyosababishwa na milipuko ya baruti sio tu huua samaki bali pia hutokomeza uhai wa matumbawe… Baada ya milipuko mara dufu kile kinachobakishwa kinakuwa tu jangwa kubwa la vifusi vya matumbawe vilivyotapakaa hapa na pale.

**Moses:** Hivi kweli milipuko hiyo ya baruti huuwa matumbawe yote?

**John:** Hata yale yalio madhubuti kabisa yalioko kwa muda mrefu sana yaliokomaa nayo huharibiwa.

**Moses:** Je matumbawe hayo yanaweza kurudia tena hali yake ya kawaida… yaani kujitengeneza upya?

**John:** Labda, lakini itachukua miaka mingi sana … pengine zaidi ya miaka mia moja. Maeneo makubwa

yaliolipuliwa yanachukua muda mrefu kujitengeneza upya kwani inakuwa vigumu kwa matumbawe kuota kwenye vitu vilivyolegea. Matumbawe madogo hujaribu kuota upya kwenye vifusi vinavyohohama hama lakini mara nyingi utakuta vinafunikwa kwa haraka na mchanga pamoja na mwani.

**Gladys:** Ina maana samaki wowote wale wa matumbawe walionusurika hutoweka kwa sababu wanakuwa wamepoteza makaazi yao?

**John:** Ndiyo sawa kabisa!

**(Hum of agreement … mguno wa makubaliano)**

**Monica:** Je kuna aina nyingine ya uvuvi ambayo pia husababisha madhara makubwa kwa mazingira ya baharini?

**John:** Ndiyo uko… na tunauita uvuvi wa kutumia kemikali ya Cyanide…

**Moses:** Watu wanatumia uvuvi huo hapa?

**John:** Hapana… hili ni tatizo lilioko zaidi barani Asia.

**(collective Oh … sauti ya Ahaaaa… ya pamoja )**

**John:** Kile kinachofanyika kwa njia hii ni kwamba wapiga mbizi huwarushia kemikali hiyo ya sumu ya Cyanide kutoka kwenye chupa samaki waliokuwa wamepumzika juu ya matumbawe. Kemikali hiyo huwashtua samaki hao lakini haiwaui na kwa njia hii huwa wanaweza kuwapata samaki hao wakiwa bado hai.

**Monica:** Lakini kwa nini wanafanya hivyo?

**Gladys:** Bila ya shaka ni kwa sababu barani Asia watu katika mikahawa hulipa fedha nyingi kuchagua samaki wanaotaka kuwala kutoka kwenye matanki ya kuhifadhia samaki wakati samaki hao wakiwa bado hai.

**Moses:** Na njia hii ya uvuvi ya kutumia kemikali hiyo ya Cyanide pia huuwa matumbawe?

**John:** Ndiyo… matumbawe pia ni viumbe hai vinayvoishi. Baya zaidi hapa ni kwamba mara nyingi samaki hujificha nyuma ya matumbawe kabla ya sumu hiyo kuanza kufanya kazi kwa hiyo wavuvi inabidi wavunje miamba pande mbili ili kuweza kuwapata samaki wao hao waliopooza… Mkiwa na muda ningelipenda kuwaonyesha mazingira mengine ya bahari yalio dhaifu.

**Fade up into SFX - SFX running outboard engine + SFX boat through water ……. sauti ya engine ya mashua na mashua ikitembea baharini**

**John:** Mikoko huwa inavutia sana. Unaikuta pale ambapo maji hujaa na kukupwa.Kwa hiyo mara nyengine kwa kiasi fulani huwa imefunkiwa na maji na mara nyengine huwa iko nje kabisa ya maji…

**SFX Engine cuts out… engine ya mashua ikizimwa**

**John:** Kuanzia hapa inabidi tutumie makasia … unaona maji jinsi yalivyokua madogo.

**SFX Paddling through water… piga makasia majini…**

**Moses:** Angalieni mizizi ya mikoko…

**John:** Mizizi hiyo huwa ina dhima maalum. Huwa inatengeneza aina fulani ya mzingile ambapo kwayo

viumbe hai viduchu sana au watoto wa viumbe hai wakubwa baharini wanaweza kuishi na kuzunguka karibu na hapo.

**Monica:** Kwa hiyo vinamasi vya mikoko ni aina ya shule ya chekekechea baharini?

**John:** Hasa! Hapa utawakuta samaki wadogo, kaa na uduvi. Mizizi ya mikoko hiyo huwapa hifadhi wanyama wadogo dhidi ya samaki wakubwa wanaokula wenzao baharini.

**Gladys:** Lakini mbona katika darasa la sayansi hivi karibuni nimejifunza kwamba vinamasi vya mikoko pia viko chini ya tishio la binaadamu…

**John:** Kwa hakika ndiyo … Na je unakumbuka kwa nini?

**Gladys:** Hapa kwa mara nyingine tena ni kosa la binaadamu. Katika baadhi ya maeneo tunazijaza ardhi sehemu hizo na kukausha kabisa maeneo hayo ya vinamasi, katika maeneo mengine mikoko hiyo inakatwa kwa ajili ya makaa pia uvuvi unakuwa wa kupidukia kwenye maeneo hayo ya mikoko.

**John:** Ni sahihi kabisa … na iwapo hatutokuwa waangalifu tutakuja kuangamiza makaazi ambayo ni muhimu kwa wanyama wadogo kuweza kukulia.

**Monica:** (sigh …… tanafusi) Inahuzunisha sana. Sijui lini tutaweza kujifunza kutunza mazingira yetu.

**(Hum of agreement ….. mguno wa makubaliano)**

**Music 0:30**

**Je ulikuwa ukijua ?**

Miamba ya matumbawe ni mojawapo ya mfumo wa ekolojia muhimu kabisa duniani. Ni maskani ya maelfu ya viumbe hai maalum na inazingatiwa na wanasayansi kuwa ni mfumo wa ekolojia mkubwa kabisa baharini wenye viumbe hai vya aina mbali mbali. Mara nyengine miamba ya matumbawe huitwa kuwa misitu ya joto baharini. Inafikiriwa kwamba miamba ya matumbawe inahifadhi zaidi ya asilimia 25 ya samaki wanaojulikana baharini. Kama vile samaki wanavyojipatia hifadhi kwenye miamba viumbe vingi hai baharini huishi ndani ya matumbawe na takriban jamii ya samaki milioni moja au viumbe vingine hai baharini wanaunda mfumo wa ekelojia wa miamba ya matumbawe.

Lakini vipi miamba ya matumbawe inakuwa? Naam kwa kutumia nishati ya jua na madini kutoka maji ya bahari matumbawe husitiri viunzi vya mawe ya chokaa ambayo hutoa makaazi na hifadhi kwa samaki na wanyama wengine wa miamba. Kurundikana kwa masimbi ya matumbawe kwa maelfu ya miaka huanzisha visiwa virefu ndani ya bahari na kuwa vikwazo vizito kuweza kuhimili dhoruba hata mawimbi makali ya tsunami.

Miamba ya matumbawe pia huzaliana sana na ni sehemu muhimu sana ya uvuvi kwa mataifa ya maeneo ya joto. Na katika maeneo ambapo utalii wa kuzamia mbizi umejikita, matumbawe huzalisha mamilioni ya dola kwa mwaka kwa uchumi wa ndani ya nchi kutokana na watalii kupiga mbizi kuangalia shani ya ufalme wa chini ya bahari.

Bila ya shaka manufaa hayo hutegemea kuwepo kwa matumbawe hai. Inasikitisha kwamba miamba ya matumbawe inatishiwa vibaya sana na harakati za binaadamu katika nchi nyingi za maeneo ya joto. Katika baadhi ya nchi inakadiriwa kwamba zaidi ya asilimia 50 ya matumbawe yameharibiwa. Kama vile tulivyosikia hivi punde tu mbinu haribifu za uvuvi kama vile kwa kutumia baruti zinahusika sana na kuangamia kwa matumbawe.

Mabadiliko ya hali ya hewa ni sababu nyengine ya kudunishwa kwa miamba ya matumbawe.Miamba mingi imeendelea kunusurika kutokana na kile wanasayansi wanachokiita kuwa uvumilivu wao wa viwango vya hali ya hewa ya joto .

Kwa hiyo ongezeko lolote lile la kupanda kwa joto husababisha hali ngumu ya kuishi kwa matumbawe. Wakati hali ya joto ikipanda matumbawe huwatimuwa viumbe hai vya kupendeza ambayvo huishi ndani yake na inakuja kupauka. Juu ya kwamba viumbe hai hivi hurudi tena kuhodhi matumbawe mara hali ya joto inaporudia kwenye viwango vya kuvumilika zaidi, kurudia tena au kubakia kwa muda mrefu katika hali ya kupauka kumethibitisha kuwa hatari kwa maisha ya baadhi ya miamba.

**Outro…… Funga kipindi…**

Na hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira kilicholenga juu ya mbinu haribifu za uvuvi na uharibifu wa miamba ya matumbawe. Kwa hiyo zingatia na kumbuka kwamba miamba ya matumbawe yetu ni makaazi kwa zaidi ya viumbe hai milioni moja baharini… lakini yanaweza kutokomezwa kwa pigo moja tu.

Ahsante kwa kuwa nasi. Iwapo unataka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaelezea marafiki zako nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be.
Kwa heri.